www.habarileo.co.tz

HABARILEO

HABARILEO GAZETI DADA LA DAILY NEWS ISSN 1821-5793 TOLEO NA. 01261 JUMAA JUNI 4, 2010 TSH. 400 KSH. 40 TANZANIA



Hatima ya Mrema Tanroads kitendawili Uk. 3

Mchakato waanza kura ya maoni Z'bar Uk. 25

Benitez hana chake Liverpool Uk. 31

CCJ si lolote?

- Wanachama 13 tu Dar ndio halali
- Uongozi wasitisha uhakiki, walia hujuma
- Tendwa ajiandaa 'kumaliza mchezo'


Na Lucy Lyatuu

PAMOJA na juhudi za Chama Cha Jamii (CCJ) kulazimisha kupewa usajili wa kudumu, jitihada hizo zinaonekana kugonga mwamba baada ya kazi ya uhakiki wa wanachama wake kugubikwa na vurugu mkoani Dar es Salaam, huku uongozi ukitangaza kusitisha kazi hiyo.

Lakini Msajili wa Vyama vya Siasa, John Tendwa anayeendesha kazi ya uhakiki huo pamoja na waterdaji wake wawili, alisema kazi hiyo itaendelea leo na kesho katika mikoa ya Pwani na Morogoro, na kama wanachama hao hawataonekana 'mchezo umekwisha.'

Kazi hiyo ya uhakiki imeingiwa na dosari baada ya jana Msajili Tendwa kusema kwa wanachama wa CCJ kwa Mkoa wa Dar es Salaam, ni 13 tu ndio halali baada ya uhakiki kati ya watu 26 waliokuwa na kadi za

Inaendelea Uk. 3



Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, John Tendwa (kulia), akijaribu kumueleweshe Mwenyekiti wa Chama Cha Jamii (CCJ), Richard Kiyabo (kushoto) wakati wa kuhakiki majina ya wanachama wa chama hicho Dar es Salaam jana ili kipewe usajili wa kudumu. (Picha na Yusuf Badi).

Magereza, RPC Barlow 'wadakwa' na Tanesco

Na Maulid Ahmed

NYUMBA zinazomilikiwa na Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Tabora, Liberatus Barlow zinadaiwa umeme wa takribani Sh milioni nne huku ofisi moja ya Magereza, Ukonga jijini Dar es Salaam, ikidaiwa inaiba umeme na kuuza kwa msikiti na maduka, operesheni ya kukata umeme ya Tanesco imebaini.

Katika operesheni hiyo ya jana Dar es Salaam ikiongozwa na Mhandisi wa Kudhibiti Mapato wa Shirika hilo, Mposheleye Mwaserga, ilibaini Magereza waliomba umeme kwa ajili ya shughuli za kufyatulia matofali, lakini badala yake umeme huo umesambazwa katika Msikiti wa Ukonga unaoonesha ulizinduliwa na Rais mstaafu Ali Hassan Mwinyi mwaka 1991.

Umeme huo pia umesambazwa kwenye maduka matano yaliyopo pembeni ya msikiti huo pamoja na vituo vya kutolea mafunzo ya kompyuta na ya kujifunza Kiingereza ambavyo vipo nyumba ya Magereza.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukuta hali hiyo ya wizi wa umeme, Mwasenga alisema wamekuta pia mita waliyoifunga imeharibika hivyo kutosoma umeme unaotumika. Inasadikiwa wateja hao wasio rasmi, wanalipa fedha kwa Ofisa Magereza ambaye hata hivyo hakujulikana jina lake wala kiwango cha fedha wanacholipa.

Hata hivyo, hawajakata huduma hiyo ya umeme.

"Tumeamua kesho (leo)

Inaendelea Uk. 3

Marufuku kusafirisha tanzanite ghafi

- Sasa kusanifiwa na kukatwa nchini
- Atakayekiuka madini kutaifishwa, leseni kufutwa

HABARI UK 3